

مِنْ  
خُرَافَةِ الشِّيَعَةِ الْغُرَابِيَّةِ  
وَالرَّدُّ عَلَيْهَا

**MIONGONI MWA UWONGO  
WA KUNDI LA SHIA (GHURAABIYYAH)  
NA MAJIBU YAKE**

Mwandishi:

**Abu Halima Arafat**

Ndugu msomaji, inafahamika kwamba Mashia wamegawika katika makundi mengi sana, mionganini mwa hayo ni kundi linaloitwa Ghuraabiyyah (kunguru), hawa ni mionganini mwa Mashia wanaoitakidi kwamba Jibril amekosea; badala ya kumpa Utume Ally Bin Abi Twalib -Allaah amuwie radhi- yeye alimpa Muhammad -swala na salamu zimshukie-!!! kwa sababu yeye Mtume amefanana sana na Ally kuliko Kunguru alivyofanana na Kunguru mwengine. Huu ni ushahidi wa maneno yao wenyewe.

**Amesema sheikh wao mkubwa Ni'matullaahi Al-Jazaairy:**

الْفُرَابِيَّةُ قَالُوا: مُحَمَّدٌ بِعَلِيٍّ أَشَبَهُ مِنَ الْفُرَابِ، وَالذَّبَابِ بِالذَّبَابِ، فَبَعَثَ اللَّهُ جِبْرِيلَ إِلَى عَلِيٍّ، فَغَلَطَ جِبْرِيلُ فِي تَبْلِيغِ الرِّسَالَةِ مِنْ عَلِيٍّ إِلَى مُحَمَّدٍ، قَالَ شَاعِرُهُمْ: (غَلَطَ الْأَمِينُ عَنْ حَيْدَرَةِ). فَيَلْعَنُونَ صَاحِبَ الرِّئِشِ يَغْنِي جِبْرِيلَ.

[Kundi la Al-Ghuraabiyyah wamesema: Muhammad ni mwenye kufanana sana na Ally kuliko Kunguru (alivyofanana) na Kunguru mwingine, na kuliko Inzi (alivyofanana) na Inzi mwingine, ndio maana Allaah alipomtuma Jibril kwenda kumpa Utume Ally, Jibril alikosea katika kufikisha Utume kutoka kwa Ally akampelekea Muhammad. Amesema mshairi wao: (Amekosea Muaminifu 'Jibril' ameacha kumpa Haidar 'Ally'). Ndio maana (wao) wanamaani Jibril 'Malaika mwenye mbawa' ]<sup>(1)</sup>.

<sup>1</sup>- Tazama: [Al-Anwaaru Nnu'maaniyyah] (Jz. 2, Uk. 208).

# بعض أوصاف الملائكة عليهم السلام في القرآن الكريم BAADHI YA SIFA ZA MALAIKA NDANI YA QUR'AN TUKUFU

## 1. Malaika ni waja wa Allaah walio tukuzwa:

﴿بَلْ عِبَادٌ مُّكَرَّمُونَ ﴾\*\* لَا يَسْقِيُونَهُ وَبِالْقَوْلِ وَهُمْ بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ ﴾

"Bali hao ni waja walio tukuzwa \*\* Hawamtangulii kwa neno na wanafanya amri zake"<sup>(2)</sup>

Amesema Ibn Kathir -Allaah amrehemu-:

"لَا يَتَقَدَّمُونَ بَيْنَ يَدَيْهِ بِأَمْرٍ، وَلَا يُخَالِفُونَهُ فِيمَا أَمْرَبْهُ بَلْ يُبَادِرُونَ إِلَى فَعْلَهِ، وَهُوَ تَعَالَى عِلْمُهُ مُحِيطٌ بِهِمْ، فَلَا يَخْفَى عَلَيْهِ مِنْهُمْ خَافِيَةٌ"

"Hawamtangulii kwa (kutenda) jambo lolote, wala hawampingi katika aliyo amrisha, bali wanaharakisha kuyafanya, na yeye Allaah elimu yake imewazunguka wao, kwa hiyo hapana siri yoyote inafichika kwake"<sup>(3)</sup>.

## 2. Malaika hawamuasi Allaah yale anayo waamrisha:

﴿لَا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمْرَهُ وَلَا يَفْعَلُونَ مَا نُهِيَّ عَنِ الْمَرْءِ ﴾

"Hawamuasi Allaah kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrisha"<sup>(4)</sup>.

Amesema Imam Al-Qurtubi -Allaah amrehemu-:

"أَيْ لَا يُخَالِفُونَهُ فِي أَمْرٍ مِنْ زِيَادَةٍ أَوْ نُقْصَانٍ. أَيْ فِي وَقْتِهِ، فَلَا يُؤَخِّرُونَهُ وَلَا يُقْدِمُونَهُ"

"Hawapingani nae katika amri zake katika kuzidisha muda wake au kupunguza, na wala hawacheleweshi (muda wake) wala hawautangulizi"<sup>(5)</sup>.

Katika Aya zilizotangulia, utaona zimetajwa baadhi ya sifa za Malaika; **wanatekeleza amri za Allaah, Hawamuasi Allaah, wanatenda wanayo amrisha.**

<sup>2</sup>- Surat Al-Anbiyaa/26.

<sup>3</sup>- Tazama: [Tafsir Ibn Kathir] (Jz. 5, Uk. 338).

<sup>4</sup>- Surat At-Tahriim/6.

<sup>5</sup>- Tazama: [Tafsirul Qurtubi] (Jz. 18, Uk. 196).

### **3. Malaika Jibril ni mjumbe Mtukufu, Mwenye nguvu na Muamunifu:**

Amesema Allaah Ta'alaa:

﴿إِنَّمَا لِقَوْلِ رَسُولٍ كَيْفَرَ \*\* ذِي قُوَّةٍ عِنْدَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ \*\* مُطَاعٌ شَهَادَةً أَمِينٍ ﴾

"Hakika hii (Qur'an) ni kauli ya Mjumbe Mtukufu \*\* Mwenye nguvu na Mwenye cheo kwa huyo Mwenye 'Arshi \*\* Mwenye kutiiwa (na Malaika huko mbinguni), tena Muaminifu"<sup>(6)</sup>.

Amesema Ibn Kathir -Allaah amrehemu- kuhusu kauli ya Allaah: ﴿أَمِينٍ ﴾

"صَفَةٌ لِجِبْرِيلَ بِالْأَمَانَةِ، وَهَذَا عَظِيمٌ جِدًا أَنَّ الرَّبَّ عَرَّوَ جَلَّ يُزَكِّي عَبْدَهُ وَرَسُولَهُ الْمَلَكِيَّ جِبْرِيلَ"

"Hii ni sifa ya Jibril kwa Uaminifu, na hili ni jambo kubwa mno, kwamba Allaah 'Azza Wajalla anamtakasa mja wake na mjumbe wake Malaika Jibril"<sup>(7)</sup>.

Jambo hili ni kujifananisha ya Mayahudi ambao walidai kwamba wanamchukia malaika Jibril, Allaah akawajibu kwamba huyo Jibril ndiye ameshuka na Qur'an kuipeleka kwenye moyo wa Mtume Muhammad -swala na salamu zimshukie:-

﴿قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ دَنَّزَهُ اللَّهُ وَعَلَىٰ قَلِيلٍ كَبِيرٌ إِذَا نَذَرَ اللَّهُ﴾

"Sema, Aliyekuwa ni adui wa Jibril, basi huyo ndiye aliye iteremsha Qur'an moyoni mwako"<sup>(8)</sup>.

Amesema Imam Al-Qurtubi -Allaah amrehemu-: "Aya hii imefahamisha juu ya heshima na utukufu wa Jibril na kuwakashifu maadui zake".

Tunamuomba Allaah atuongoze njia ya sawa.

Abu Halima Arafaat

Jumatatu 17/5/1444H – 11/12/2022M

Pongwe tanga

<sup>6</sup>- Surat At-Takwir/19-21.

<sup>7</sup>- Tazama: [Tafsir Ibn Kathir] (Jz. 8, Uk. 339).

<sup>8</sup>- Surat Al-Baqara/97.